

Maana ya Majilio

Na Mchg. Thomas Maumbuka

'Majilio; ni neno la Kilatini lenye maana ya "kuja" au "kufika" (adventus) - hasa kuja kwa kitu ambacho kina umuhimu mkubwa na wa kipekee. Kipindi cha majilio huanza majuma manne kabla ya Sikukuu ya Krismas, Disemba 25 au siku ya kukumbuka kuzaliwa kwa Yesu Kristo ambayo huwa ni Jumapili iliyo karibu na Novemba 30 na kuishia Disemba 24.

Kwa Kanisa letu la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Majilio ndio mwanzo wa Mwaka Mpya wa Kanisa. Mkazo mkubwa katika kipindi hiki ni kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu Kristo siku ya Krismasi na matazamio ya kurudi kwa Yesu Kristo Mfalme mara ya pili.

Majilio ni kipindi cha maandalizi ya kiroho ambapo wakristo wanajiandaa kukumbuka kuzaliwa kwa Yesu Kristo au kuja kwa Mfalme siku ya Krismasi. Hivyo wanapaswa kuelekeza mioyo na mawazo yao kumngoja Yesu kuja mara ya pili kulichukua Kanisa. Kwa maana hii, majilio ni kipindi cha mashangilio na matumaini ya kiimani.

Kusudi la Kanisa kuadhimisha au kuwa na kipindi cha majilio cha kumngoja Bwana si tu kwa kumshukuru Mungu kwa ukombozi, kwa kuzaliwa kwa Yesu Kristo au kuja kwa Yesu Kristo duniani kwa mara ya kwanza kama mwanadamu, bali pia kwa uwepo wake katikati yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, na matarajio makubwa au matumaini makubwa ya kuja kwa Yesu mara ya mwisho kulinyakua Kanisa.

"Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu..." (Zak. 9:9b). Nia ya kipindi hicho ni kuwakumbusha Wakristo kupata nafasi ya kutafakari Neno la Mungu kwa pamoja na pengine kwa kupitia vifungu maalumu katika Biblia. Ni kipindi cha kuweka mkazo katika sala na maombi pamoja na kutubu kukifuatiwa na matarajio ya matumaini ya furaha ya ukombozi.

Sababu nyingine ni ili kuwavuta Wakristo karibu zaidi na Mungu wao kwa njia ya mafundisho, nyimbo za mashangilio na Liturgia hasa katika kipindi hicho cha mapumiziko ya kazi za kila siku ambapo kwa wengi ni kipindi cha likizo; hivyo kusahau taabu, hofu na changamoto za maisha ya kila siku na kuelekeza mawazo yao kwa Yesu Kristo mkombozi wao.

Katika Kitabu cha Tumwabudu Mungu Wetu Wimbo Namba 10, ubeti wa 1 una maneno haya: "Bwana anakuja twendeni kumlaki Bwana Mungu wa majeshi, lwasheni mioyo tukampokee Huyo mwenye utukufu. Karibu Bwana, njoo. Karibu Bwana, njoo. Shinda pamoja nasi.

Lakini si hivyo tu, bali majilio ni kipindi cha kila Mkristo kwa maisha yake binafsi kujitoa na kupata faragha na Mungu wake kwa kusoma Neno la Mungu kila siku, kutoa muda wa ziada kwa maombi ya binafsi, familia, Kanisa na taifa; kuwatembelea majirani na kuwatia moyo ili kumngoja Yesu Kristo hasa kwa walio kata tamaa; kuwatembelea wagonjwa na wasiojiweza na kushiriki pamoja nao katika maombi na hata ikiwezekana kuwasaidia wahitaji.

Majilio si kipindi tu cha maandalizi ya kihistoria ya kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu Kristo siku ya Krismasi, bali ni mwanzo wa kuadhimisha muujiza wa Mungu kufanyika mwanadamu (incarnation) kwa njia ya ajabu mno na kisha kukaa pamoja nasi.

Kuja kwa Yesu Kristo kulitabiriwa tangu zamani na manabii wa Agano la Kale: “Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa tumepewa mtoto mwanamume na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake, naye ataitwa jina lake mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele mfalme wa amani” (Isa 9:6).

Pia “Furahi sana Ee binti sayuni, piga kelele Ee binti Yerusalemu tazama mfalme wako anakuja kwako” Zek 9:9. Kanisa linakumbushwa kwamba linaishi katikati ya vipindi viwili vya kihistoria: kuja kwa Yesu Kristo kwa njia ya mwili (flesh) duniani na kuja kwa utukufu siku ya mwisho kulinyakua kanisa.

Hivyo kanisa linapaswa kuwa imara katika imani hasa tunapongojea kwa furaha na matumaini kuja kwa mwokozi wetu Yesu Kristo. Utawala wa Mungu uko katikati yetu lakini bado haujafunuliwa katika ukamilifu wake.

Wakristo tunaadhimisha kile ambacho tayari tunacho lakini wakati huo huo tukitaraji kile kitachofunuliwa baadaye kwa ukamilifu kama anavyosema Mtume Paulo kwamba sasa tunaona kwa kioo lakini tutaona uso kwa uso.

Kipindi cha majilio sisi tulio wakristo tutegemee kufanywa au kuumbwa upya mioyo yetu na kuwa tayari kumpokea Yesu Kristo kwa upya mioyoni mwetu, kutengeneza maisha yetu, kugeuka na kuacha njia mbaya na kuweka ukristo wetu katika vitendo na si katika maneno tu. Nyakati hizi ujumbe muhimu wa majilio ni ‘tubuni kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia’.

(Wasiliana na Mchg. Maumbuka kwa sms: +255 777 6842 440).